OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MLIMBA.

SHULE YA SEKONDARI MASAGATI,

S.L.P 123,

MLIMBA.

20/12/2021

Ndugu ……..

S.L.P …….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KWA MWAKA 2021.

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa wewe ndugu ……. mwenye namba ……. ambaye umesoma shule ya msingi ……iliyopo kata ya Masagati, wilaya ya Mlimba. Umechaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari kidato cha kwanza (I) katika shule ya Sekondari Masagati kwa mwaka 2021. Hongera sana kwa kuchaguliwa kwako.

Shule itafunguliwa tarehe 09/01/2021 siku ya jumatatu, Hivyo unapaswa kufanya maandalizi yanayotakiwa mapema na kufika siku hiyo kwani hapatakuwa na visingizio vingine kwa sababu. Hakuna fedha yeyote ile utakayo tozwa kwa ajili ya kujiunga na masomo ya sekondari kama agizo la serikali linavyoagiza.

Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wazazi/ mlezi ambaye hatamfikisha mwanae shuleni siku ya kufungua shule na baada ya wiki moja kupita atafikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Ninakutakia kila la heri katika maandalizi muhimu na karibu sana katika shule yetu ya Sekondari Masagati, kwa tarehe na siku iliyotajwa hapo juu bila kukosa ili kuepuka adhabu zisizostahili na ambazo kwa mzazi/ mlezi zinazuilika kabisa. Nakuomba timiza wajibu wako.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978, zifuatazo ni sheria za jumla za shule hii
   i. Heshima kwa walimu, viranja, wazazi na wanafunzi wengine ni jambo la lazima
   ii. Mahudhurio mazuri darasani na nje ya darasa ni mhumu
   iii. Kuwahi mapema shuleni, darasani na katika kila shughuli utakayopewa ni jambo la lazima.
   iv. Kufahamu mipaka shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje na mipaka ya shule ni jambo la mhimu kwa kila mwanafunzi.
   v. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule .
   vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
   vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
   viii. Uvaaji sahihi wa sare za shule ikiwa ni pamoja na kuchomekea pamoja na kuvaa tai ya shule muda wote.
   ix. Lugha ya mazungumzo katika shule hii ni lugha ya kiingereza. Lugha ya Kiswahili itatumika wakati wa kipindi cha somo la Kiswahili tu.

SHERIA ZA SHULE

2. Makosa yanayopelekea mwanafunzi afukuzwe shule ni :-
   i. Wizi.
   ii. Uasherati, ubakaji na ushoga.
   iii. Uvutaji wa bangi na sigara.
   iv. Makosa ya jinai.
   v. Kupiga au kupigana.
   vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
   vii. Kudharau bendera na wimbo wa taifa.
   viii. Kuoa au kuolewa.
   ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
   x. Kutoa mimba.
   xi. Kugoma, kuchochea, kuongoza na kuvuruga usalama wa watu shuleni.
   xii. Kukataa adhabu ya mwalimu au kiranja kwa makusudi.
   xiii. Kushikwa na simu shuleni.
   xiv. Kaka porini wakati wa vipindi au wakati wa shughuli yoyote hapa shuleni.
   xv. Utoro sugu.

MAELEKEZO MUHIMU KUHUSU SHULE KWA MWAKA 2021

1. **SARE ZA SHULE**

A. WAVULANA

i. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi (Tetroni) yasibane na yasiwe na urembo wowowte ule.
ii. Suruali mbili (2) zisibane za rangi ya Dark Blue zenye marinda mawili na turn up (Pata maelezo shuleni kabla ya shule kufunguliwa kwa ufafanuzi zaidi).
iii. Viatu vyeusi vya kamba ambavyo vinang'arishwa na kiwi na visivyo na visigino virefu
iv. Soksi nyeusi za kutosha kuanzia jozi mbili (2)
v. Tai ya rangi ya Dark blue inayofanana na suruali
vi. Mkanda mweusi wa ngozi
vii. T – shirt moja (pata maelezo shuleni kabla ya shule kufunguliwa kwa ufafanuzi zaidi)
viii. Viatu (raba) vya michezo.
ix. Traki suti nyeusi yenyemikanda myeupe, bukta nyekundu au njano kwa ajili ya michezo.

B. WASICHANA

i. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi (Tetroni) yasibane na yasiwe na urembo wowote ule.
ii. Sketi mbili (2) zisibane za rangi ya Dark blue ndefu zenye heshima na iliyovuka magoti (pata maelekezo shuleni kabla ya shule kufunguliwa kwa ufafanuzi zaidi)
iii. Viatu vyeusi vya kamba ambavyo vinang'arishwa na kiwi na visivyo na visigino virefu.
iv. Soksi nyeupe za kutosha kuanzia jozi mbili.
v. Tai ya rangi ya kijani iliyofanana na sketi
vi. Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule (pata maelekezo shuleni)
vii. T – shirt moja (pata maelekezo shuleni kabla ya shule kufunguliwa kwa ufafanuzi zaidi)
viii. Viatu (raba) vya michezo
ix. Truki suti nyeusi yenye mikanda myeupe kwaajili ya michezo

NB* Nywele ni sehemu ya sare ya shule, zinatakiwa ziwe fupi za kuchana, aidha kuchana ziwe fupi na safi wakati wote. Hairuhusiwi kuvaa bangili (kacha) mapambo ya aina yoyote ili shuleni.

2. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA SHULE.

a) Daftari kubwa (counter books) kumi (10) na kalamu za kutosha.

b) Kwa ajiri ya kukuza hali yetu ya usafi wa mazingira ya shule, mwanafunzi atapaswa kuja na fagio chelewa.

Ni mhimu kutekeleza haya ili kuweka mazingira ya shule yetu kuwa safi na salama muda wote kwani uwepo wa mazingira safi na salama ndio kichocheo chanya cha ujifunzaji na ufundishaji.

NB: siku ya kufungua shule kutakuwa na kikao wazazi wote wa wanafunzi wa kidato cha kwanza 2021 kwa lengo la kuwaandikisha wanafunzi pamoja na kupewa maelekezo mengine ya shule. Tafadhari wazazi wa wanafunzi wa kidato cha kwanza 2021 fikeni bila kukosa.

Nawatakia maandalizi mema na karibuni sana Masagati Sekondari.

_____

STANLEY .N. MWINUKA

MKUU WA SHULE

KIAMBATISHO A.

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASAGATI

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mwanafunzi ajaze sehemu hii

1. Mimi _____ ninakubali kujiunga na shule ya sekondari Masagati katika kidato cha **kwanza.**
2. Mimi nitakapo kuwa mwanafunzi wa Masagati Sekondari , ninakubali kwamba:-
   i. Nitafika shuleni siku ya kufungua shule bila kuchelewa.
   ii. Nitatii sheria zote za shule pamoja na kutoshiriki katika ulevi, migomo na migogoro ya aina yoyote na nitahudhuria vipindi vyote vya darasani na kazi za nje kwa mujibu wa ratiba ya shule.
   iii. Nitatumia juhudi na maarifa yote kujielimisha kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vipindi pamoja na kufanya mazoezi na mitihani yote.

Saini ya mwanafunzi _____ tarehe _____

B. SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI

Mzazi/mlezi ajaze sehemu hii

1. Mimi _____ nimekubali mtoto wangu ajiunge na shule ya Secondary Masagati
   Ninaomba kwamba:-
   i. Nitawasaidia walimu kumlea mwanangu kitaaluma na kitabia.
   ii. Nitamuonya na kumsisitiza mwanangu kutii sheria za shule.
   iii. Nitahakikisha mwanangu anafika shule kila siku pale anapohitajika.
   iv. Nipo tayari kuwajibika kwa jambo lolote atakalo fanya mwanangu ambalo ni kinyume na sheria za shule. Ambalo litaonekana limesababishwa na uzembe wangu mimi mzazi.

Anwani yangu ya kudumu

Namba ya simu _____ kijiji _____

Sahihi ya mzazi/ mlezi _____

(Tafadhari njoo na fomu hii unapokuja shuleni ikiwa imejazwa)

KIAMBATISHO B

MASAGATI SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical officer in respect of all form entrants

1. Student's name ……..
2. Age …… sex ……...
3. Blood count ……..
4. Stool examination ……
5. Syphilis or venereal diseases test …….
6. T.B test …….
7. Eye test …….
8. Ears test ……
9. Spleen ……
10. Abdomen ……

ADDITIONAL INFORMATION

If any physical impairment, infection, chronic or family disease …….....

……
…….

I CERTIFY THAT ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTER STUDIES IN EDUCATION

Station …… signature …….

Date …… designation

NB. Tafadhari taarifa hii ijazwe na tabibu aliyeidhinishwa katika hospitali ya serikali tu.

(Fomu hii irejeshwe siku ya kuripoti shuleni ikiwa imejazwa)